MWANANCHI
Jumatano machi 4, 2026

# MAONI & U

## Nukuu



Watu dhaifu kamwe hawawezi k
na watu thabiti.

**Mahatma Gandhi, mpigania uhu**

# Bodaboda zisiachwe kuwa janga

Sekta ya usafiri wa pikipiki, maarufu kama bodaboda, imekuwa mhimili muhimu wa usafirishaji na uchumi nchini Tanzania. Kwa vijana maelfu, hii ni ajira; kwa mwananchi wa kawaida, huu ni usafiri wa haraka unaopenya foleni nzito za majiji kama Dar es Salaam na kufika kule ambako daladala haliwezi kukanyaga.

Hata hivyo, hali ya ukaidi wa sheria inayozidi kukithiri barabarani ni ishara ya wazi kuwa tusipochukua hatua madhubuti sasa, sekta hii inageuka kuwa janga la kitaifa.

Takwimu za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) zinaonyesha ongezeko kubwa la leseni za bodaboda kwa asilimia 44.5 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ongezeko hili la vyombo barabarani halijaambatana na ongezeko la nidhamu.

Badala yake, imekuwa ni kawaida kushuhudia uvunjifu wa Sheria ya Usalama Barabarani (Sura ya 168), hususan Kifungu cha 70 kinachokataza kupakia abiria zaidi ya mmoja maarufu kama mshikaki na Kifungu cha 45(12) kinachomtaka dereva na abiria kuvaa kofia ngumu.

Ni jambo la kusikitisha kuwa "mshikaki" sasa umekuwa mfumo rasmi wa biashara katika maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam. kwa wanafunzi ndio usiseme, hao wanabebwa kuanzia watatu hadi wanne.

Madereva wanaona kubeba abiria wawili kwa mpigo ni njia ya haraka ya kufikisha malengo ya kifedha ya Sh20,000 kwa siku. Hoja hii ya kiuchumi haina mashiko mbele ya thamani ya uhai wa Mtanzania. Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa vifo vitokanavyo na ajali za pikipiki viliongezeka kwa asilimia 13.3 ndani ya mwaka mmoja pekee (2022-2023).

Hii ni ishara kuwa ingawa ajali zinaweza kupungua kidogo, madhara yake yanazidi kuwa makubwa na ya mauti.

Changamoto ya uvaaji wa kofia ngumu imekuwa ikigubikwa na visingizio vya mitindo ya nywele kwa wanawake na hofu ya usafi. Ni lazima tufike mahali tukatae kuwa "nywele si heri kuliko fuvu la kichwa kupasuka." Hata hivyo, mamlaka zinaweza kuiga mfano wa nchi jirani ya Rwanda kwa kuanzisha utaratibu wa matumizi ya karatasi laini (disposable hair nets) za kuvaa kichwani kabla ya kofia ngumu ili kuondoa hofu ya magonjwa ya ngozi. Huu ni ubunifu mdogo unaoweza kuokoa maisha mengi.

Aidha, kuna mkanganyiko wa kisheria unaopaswa kutatuliwa. Wakati Latra ikisisitiza kuwa bodaboda ni usafiri wa kukodi na si wa kukusanya abiria vituoni kama daladala, uhalisia mitaani ni tofauti.

Bodaboda na bajaji wanafanya kazi kama daladala ndogo, wakipoka soko la usafiri wa umma na kusababisha uvunjifu wa amani barabarani. Madereva wa daladala wanalalamikia ushindani usio wa haki na fujo zinazofanywa na bodaboda mbele ya macho ya askari.

Hatuwezi kuendelea kuangalia upande mmoja wakati vijana wetu wanapoteza nguvu kazi na abiria wakibaki na ulemavu wa kudumu. Jeshi la Polisi na Latra lazima waache kutoa elimu pekee na kuanza kuchukua hatua kali za kisheria bila kumuonea mtu haya. Sheria msumeno; lazima ikate pande zote.

Lakini zaidi ya yote, abiria mna nafasi kubwa. Usalama wako huanza na wewe. Kukataa kupandishwa mshikaki, kukataa kuendeshwa kwa kasi ya ajabu, na kusisitiza kuvaa kofia ngumu ni haki yako ya msingi. Usikubali kuweka rehani uhai wako kwa sababu tu ya kuwahi dakika kumi kazini. Bodaboda zisiachwe ziendelee kuwa mashine za kifo; zibaki kuwa chombo cha maendeleo.

Habarileo Jumatano Machi 4, 2026 Pg 2

# SGR kubeba mizigo Dar mwezi huu

Na Zena Chande

SERIKALI imesema mwishoni mwa mwezi huu treni ya kisasa (SGR) inatarajiwa kuanza kusafirisha mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Dodoma.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema hayo wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa matangi 15 ya mafuta Kigamboni Dar es Salaam jana.

Profesa Mbarawa alisema miradi kwenye sekta ya uchukuzi imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

"TRC (Shirika la Reli Tanzania) nayo kwa kutumia SGR imeanza kutoa huduma ya mizigo kutoka stesheni ya Pugu Dar es Salaam hadi Ihumwa Dodoma na mwishoni mwa mwezi huu itaanza kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenye eneo maalumu lililojengwa na kupelekwa Dodoma," alisema.

Profesa Mbarawa alisema wizara inajipanga kuanzisha matumizi ya bandari kavu Morogoro, Dodoma na Shinyanga.

"Tunakushukuru (Rais Samia) kwa kuipa kipaumbele sekta ya uchukuzi na kutupatia fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ukiwemo mradi huu... utekelezaji wa mradi huu utaifanya Tanzania kuendelea kuaminika zaidi na wadau wa sekta ya usafirishaji na usambazaji na kufungua soko la kibiashara la kimataifa," alisema.

Aidha, alisema Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikiana na wizara na taasisi nyingine katika kuhakikisha mnyororo mzima wa thamani unazingatiwa.

Alisema wizara imejikita kuunganisha huduma na kuboresha mifumo ya uendeshaji inayowezesha bidhaa, mizigo na usafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila kuchelewa.

Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu alimuomba Rais na serikali yake kujenga mitambo ya kusafisha mafuta.

"Mitambo hii chini ya uongozi wako itaweza kuhudumia ukanda wote huu ambao hawana bahari na wana shida kupata mafuta... tutumie changamoto ya sasa duniani kuipaisha Tanzania kiuchumi... na tukifanikiwa mradi huu tufanye mradi wa lami na miradi mingine na uchumi wetu utakua," alisema Zungu.

Aliongeza: "Leo (jana) tumezindua matangi kwa maslahi mapana ya taifa letu, kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa sasa duniani, athari ya mafuta itajitokeza lakini umeamua (Rais Samia) kuhakikisha kwetu isijitokeze... nakupongeza kwa hilo Rais".

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara alisema serikali inawekeza kimkakati katika sekta ya uchukuzi.

Profesa Kahyarara alisema hayo wakati akizungumza kwenye kipindi cha Jambo Tanzania kilichorushwa na TBC1 jana asubuhi.

"Tukiangalia katika bandari tuna uwekezaji mkubwa umefanyika katika bandari, tumeona mageuzi makubwa katika uendeshaji wa bandari, vitu vyote ambavyo vimekuwa na tija kubwa na tunaona fedha ambazo zinakusanywa na TRA zimeongezeka sana," alisema.

Profesa Kahyarara alisema katika maeneo yote ambayo Reli ya Kisasa (SGR) inapita, asilimia 80 ya mizigo itabebwa na treni.

"SGR ina uwezo wa kubeba tani milioni 25, ina maana mzigo wote unaokwenda nje ya nchi tunakuwa tumeumaliza, tunaanzia kwamba malori yakitoka huko yanakotoka yaishie Morogoro, yaishie Isaka na sisi tutawafuata huko na treni watakuta mizigo yao na kuipeleka huko iendako," alisema.

CamScanner

 Uhuru Jumatano Machi 4, 2026 Pg 8



**BASI** la Daladala linalofanya safari zake kati ya Mbezi na Mbagala likiwa limejaza abiria kupita kiasi kinyume cha sheria za usalama barabarani, katika Barabara ya Nelson Mandela, Dar es salaam, juzi. (Picha na Christopher Lissa).

CamScanner

Raia Mwema Jumatano Machi 4, 2026 pg 5

# Ujenzi wa SGR washika kasi

**Na Mwandishi Wetu**

**HADI** Desemba mwaka jana, utandazaji wa Reli ya Kisasa (SGR), inayosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC), umefikia kilometa 747, sawa na asilimia 61 ya lengo la kilometa 1,219 za mwaka 2025/26.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akijibu swali la mwandishi wa habari hizi aliyetaka kujua hali ya utekelezaji wa ujenzi wa reli hiyo.

Msigwa alisema ujenzi wa SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam-Mwanza yenye kilometa 1,219 za njia kuu na kilometa 377 za njia za kupishana umefika hatua mbalimbali.

Alitaja vipande hivyo kuwa ni Dar es Salaam-Morogoro kilometa 300 ambayo ujenzi umekamilika kwa asilimia 99.93; Morogoro-Makutupora kilometa 422, asilimia 98.6; Makutupora-Tabora kilometa 368, asilimia 14.54; Tabora-Isaka, kilometa 165, asilimia 8.95; Mwanza-Isaka, kilometa 341, asilimia 67.85 na Tabora-Kigoma kilometa 506, asilimia 9.06.

Alisema kipande cha kuingia bandarini kimefikia asilimia 99.93, jambo litakaloongeza chachu ya kutumia bandari kavu ya Kwala mkoani Pwani. Aliongeza kuwa kukamilika kwa SGR kumepunguza muda wa safari ya Dar es Salaam-Dodoma kutoka saa 1,012 kwa mabasi hadi saa 34 kwa treni.

"Tangu kuanza huduma hadi Desemba mwaka jana, abiria 4,665,004 walisafirishwa, tani 52,305 za mizigo zimesafirishwa, Watanzania 207,468 wameajiriwa, ajira 1,304 kwenye vituo vya SGR, 55,284 za moja kwa moja na 150,880 zisizo za moja kwa moja.

"Huduma ya SGR imeongeza tija kiuchumi, kibiashara na kiutalii, hususan kwa wasafiri wanaokwenda hifadhi za Mikumi, Ruaha na Udzungwa.

Mwaka 2024/25 na nusu ya 2025/26, Wizara ya Uchukuzi imekamilisha upembuzi yakinifu wa reli za mijini Dar es Salaam na Dodoma, hatua iliyowezesha kupatikana fedha za msaada kwa ajili ya usanifu wa kina.

"Tangu Desemba mwaka jana, TRC ilianza kujiendesha bila ruzuku ya mishahara ya takribani Sh bilioni 13 kwa mwaka iliyokuwa ikitolewa kwa takribani miaka 13," alisema.

Aidha, TRC imeanzisha kampuni tanzu ya Tanzania Railway Limited inayoimiliki kwa asilimia 100 ili kuongeza ufanisi kibiashara na kimapato.

Alisema Serikali imeendelea kuboresha reli ya zamani (MGR) kwa kuondoa reli za ratili 45 na kuweka za ratili 80, kuongeza uwezo wa madaraja kutoka ekseli 13.5 hadi 18.5 na kusaini mkataba wa ukarabati wa kipande cha Tabora-Kigoma kilometa 411.

Msigwa alisema hadi Juni mwaka huu, TRC inakusudia kuwa na vitendea kazi 59 ambavyo ni vichwa na mabehewa.

Hatua zilizochukuliwa ni MGR kununua mabehewa 100 ya mizigo, vichwa vinane na viwili tayari vimewasili na viko kwenye majaribio na uundwaji wa vichwa sita kwenye karakana ya Pugu utakaokamilika mwezi huu.

"Kwa Reli ya SGR vichwa 17 vya umeme, seti 10 za treni za umeme, mabehewa 89 ya abiria, mitambo ya matengenezo 24, mabehewa 1,430 ya mizigo vimenunuliwa na 264 ambapo hadi Desemba mwaka jana vilishawasili," alisema.

Alisema pia walikarabati vichwa tisa vya treni, mabehewa 37 ya abiria na 368 ya mizigo.

Aidha, alisema Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imepiga hatua kubwa ya kufufua Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na mkataba wa ufufuaji na uboreshaji wa reli hiyo ulisainiwa Septemba 29 mwaka jana kati ya serikali za Tanzania na Zambia kwa kushirikiana na kampuni ya CCECC ya China.

CamScanner